**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO**

*(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)*

Kumb.Na.MDC/L.20/12/32 Tarehe 25/02/2022**.**

---

**YAH. TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI YA MAKAZI NA POSTIKODI.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda kwa nafasi za kukusanya taarifa kwenye zoezi la Anwani za makazi katika kata na vijijini na vitongoji vya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

**A: SIFA ZA WAOMBAJI.**

i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-40
ii. Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
iii. Awe anamiliki simu janja Adroid yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima.
iv. Awe na Barua pepe (email address) na nywila (password) inayofanya kazi.
v. Awe na uwezo wa kusoma ramani za mitaa
vi. Awe ni mkazi wa kata husika.

**B: KAZI NA MAJUKUMU.**

i. Kukusanya taaarifa za nyumba, Viwanja, na Makazi ya huduma kwa kutumia mfumo wa Anwani za makazi.
ii. Kuandika namba za nyumba, Viwanja na maeneo ya huduma.
iii. Kutuma data kwenye mfumo wa Anwani za makazi.
iv. Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku (10).
v.

**C: MAOMBI YAAMBATANISHWE NA.**

- Nakala ya cheti cha kidato Nne na kuendelea
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- Picha 2 (Passport size).

**D: JINSI YA KUTUMA MAOMBI:**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na Anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu, barua pepe. Barua ziwasilishwe Ofisi za kata uliopo au ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Mvuha kwa Mkono na siyo kwa Posta kwa anwani ifuatayo:

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
Barabara ya Bigwa – Kisaki (Mvuha)
S.L.P 1880
**Morogoro.**

Simu: +255 23 2613185
Nukushi: 023 261 3185
Barua Pepe: ded@morogorodc.go.tz
Tovuti: www.Morogorodc.go.tz

**E: MALIPO:**

Malipo kwa kazi ni 30,000.00 kwa siku.

**F: TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 02/03/2022

Rehama S. Bwasi

**Mkurugenzi Halmashauri Wilaya**

**MOROGORO**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
MOROGORO DISTRICT COUNCIL